

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 022 2126826  
Nukushi: 022 2126834  
Tovuti: [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz)  
Baruapepe: [km@habari.go.tz](mailto:km@habari.go.tz)



S. L. P. 25,  
Mtaa wa Habari,  
Mji wa Serikali Mtumba  
40481 DODOMA.

### TAARIFA KWA UMMA

### SALAMU ZA POLE

**Desemba 25, 2020 – Dar es Salaam**

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) amepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) Bw. Godfrey Mngereza kilichotokea Desemba 24, 2020 katika Hospitali Kuu ya Mkoa Dodoma alipokuwa anapatiwa matibabu.

“Kwa muda mrefu tumekuwa mashuhuda wa namna alivyoweza kusimamia maslahi ya kazi za Sanaa na wasanii, hakuwa mtu wa kukaa ofisini tu, alizunguka kwenye matukio yote muhimu yanayoihusu Sanaa yawe yameandaliwa na Serikali, taasisi kubwa au hata wasanii wa kawaida. Alikuwa mwepesi wa kutoa ushauri na nasaha mara kwa mara. Ni pigo tumepoteza mtu muhimu sana” alisema Bashungwa.

Marehemu Mngereza atakumbukwa kwa umahiri wake wa kuisimamia Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa ya mwaka 1984 na Kanuni zake na uwezo wake wa kusimamia maadili katika kazi za Sanaa pamoja na kuifahamu sekta kwa mapana yake hatua iliyosaidia kukuza maendeleo na utengenezaji wa kazi za Sanaa nchini.

Waziri Bashungwa ametoa pole kwa familia, watumishi wa Wizara, taasisi ya BASATA, wasanii, wadau wote wa tasnia ya sanaa, ndugu, jamaa na marafiki. Pia anawaomba wote kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, wapate nguvu, ujasiri na moyo wa ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.

Imetolewa na

Eleuteri E. Mangi

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,  
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.**